JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA KOROSHO TANZANIA



# JARIDA LA KOROSHO MWEZI APRILI 2023



TOLEO NA.CBT 008

IMEANDALIWA NA

BODI YA KOROSHO TANZANIA





## 1.0. UTANGULIZI

Msimu wa Korosho Nchini Tanzania unakaribia kufikia tamati baada ya mikoa ya Tanga, Dodoma na Singida kumaliza mauzo mwezi Aprili.

Shughuli ya utoaji wa vibali vya kusafirisha Korosho ghafi nje ya nchi inaendelea ambapo hadi sasa zaidi ya tani 168,971.063 za korosho ghafi zenye thamani ya Dola za Kimarekani 155,734,734.67 (FOB Value) zimeombewa vibali vya kusafirisha nje ya nchi. Pia vibali vya kusafirisha korosho karanga vinaendelea kutolewa na hadi sasa zaidi ya tani 1,870.118 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 51,645,723.88 (FOB Value) zimesafirishwa.

## 2.0. MWENENDO WA SOKO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI


### 2.1. MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

Nchini Ivory Coast, kutokana na kuendelea kwa mvua ubora wa korosho unazidi kushuka na wakulima bado hawakaushi korosho zao kwa kiwango kinachohitajika hali inayopelekea kuzidi kushuka kwa bei. Bei ya wastani kwa mkulima imeshuka kutoka Dola za Kimarekani 0.56 hadi 0.42 kwa kilogramu. Wabanguaji wanafurahia kushuka kwa bei kwa sababu wataweza kupata malighafi ya viwanda vyao kwa bei ya chini ingawa bei iliyopangwa na serikari kwa korosho zinazonunuliwa na viwanda vya ndani ni Dola za kimarekani 0.62 kwa kilogramu.

Nchini Ghana mauzo ya korosho yanaendelea kukiwa na mahitaji madogo, ubora wa korosho pia ni wa wastani na bei kwa mwezi April imeshuka kutoka dola za kimarekani 0.69 - 0.73 mwezi Machi hadi Dola za Kimarekani 0.47 - 0.51 mwezi Aprili. Msimu wa uzalishaji unakaribia kuisha, kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 inakadiriwa kiasi cha tani 260,000 hadi 300,000 zimeuzwa (inajumuisha korosho zilizoingia kutoka nchini Ivory Coast). Hadi sasa Ghana imeuza nje zaidi ya tani 136,000 za korosho ghafi.

**Jedwali Na. 1: Usafirishaji wa Korosho Ghafi kutoka Ghana Kwenda Nchi Mbalimbali Kuanzia Januari hadi Machi, 2023**

| USAFIRISHAJI WA KOROSHO GHAFI GHANA KWENDA NCHI MBALI MBALI KUANZIA JANUARI 2023 HADI MACHI 2023 | | | |
|---|---|---|---|
| NA. | NCHI | KIASI (TANI) | THAMANI (USD) |
| 1 | Brazil | 100.00 | 100,171.00 |
| 2 | China | 105.00 | 110,479.00 |
| 3 | India | 107,165.00 | 111,425,679.00 |
| 4 | Morocco | 226.00 | 236,718.00 |
| 5 | Singapore | 190.00 | 194,712.00 |
| 6 | Umoja wa Falme za Kiarabu | 604.00 | 586,055.00 |
| 7 | Vietnam | 26,458.00 | 27,141,961.00 |
| 8 | Nyinginezo | 1,759.00 | 1,809,379.00 |
| | **Jumla Kuu** | **136,607.00** | **141,605,154.00** |




**Chanzo:** Cashewnutinformation

Nchini Benin pamoja na ubora mzuri wa korosho zake bado mauzo yapo chini kutokana na sera ya nchi ya kutaka viwanda vya ndani pekee ndivyo vinunue korosho ghafi kwa sasa na viwanda vingi havina fedha za kutosha kununua mzigo wote. Kumekuwa na hofu ya usafirishaji haramu wa korosho ghafi kwenda nchi jirani ya Togo lakini Serikari inachukua hatua kuzuia udanganyifu huo kwa kutumia jeshi kuchimba mitaro maeneo ya mipakani (Savalou-Tchetti) ili kuzuia magari ya aina yoyote kupita bila ruhusa.


Nchini Burkina Faso mauzo yanaendelea na hakuna mabadiliko makubwa ya bei huku serikali ikiendelea na msimamo mkali juu ya kuheshimu sera ya bei ya chini. Bei ya korosho kwa mkulima ni kati ya Dola za Kimarekani 0.47 hadi 0.50 kwa kilogramu na bei ya malipwani (FOB Value) ni kati ya Dola za Kimarekani 950 hadi 1,050 kwa tani.

### 2.2. Hali ya Soko la Korosho Nchini India

Bei za korosho ghafi ambazo zilikuwa zimepanda na kuwa Dola za Kimarekani 1.52 hadi 1.58 kwa kilogaramu mwezi Machi zimeshuka na kufikia Dola za KImarekani 1.40 kwa kilogramu. Mahitaji ya korosho karanga kwa soko la ndani bado sio ya kuridhisha na mauzo ya nje pia ni ya chini na hakuna mahitaji ya korosho karanga kwa madaraja ya juu kama W210 na W240 ingawa kuna kiasi kidogo cha mahitaji kwa daraja la W320.

**Jedwali Na.2: Korosho Ghafi Zilizoingia India Kutoka Nchi Mbalimbali Kwa Mwezi Machi, 2023.**

| KOROSHO GHAFI ZILIZOINGIA INDIA KUTOKA NCHI MBALIMBALI KWA MWEZI MACHI 2023 | | |
|---|---|---|
| NA | NCHI | KIASI (TANI) |
| 1 | Tanzania | 4,774 |
| 2 | Benin | 1,191 |
| 3 | Ivory Coast | 2,142 |
| 4 | Guinea Bissau | 1,600 |
| 5 | Guinea | 626 |
| 6 | Burkina Faso | 1,000 |
| 7 | Senegal | 212 |
| 9 | Ghana | 29,451 |
| 10 | Nigeria | 54 |
| 13 | Togo | 115 |
| 14 | Msumbiji | 9,076 |
| | **Jumla Kuu** | **50,241** |





**Chanzo:** Cashewnutinformation



**Jedwali Na. 3: Usafirishaji wa Korosho Karanga India Kwenda Nchi Mbalimbali Kwa Mwezi Machi 2023.**

| USAFIRISHAJI WA KOROSHO KARANGA INDIA KWENDA NCHI MBALIMBALI KWA MWEZI MACHI 2023 | | |
|---|---|---|
| **NA** | **NCHI** | **KIASI(TANI)** |
| 1 | Umoja wa Falme za Kiarabu | 1,338 |
| 2 | Saud Arabia | 562 |
| 3 | Uholanzi | 556 |
| 4 | Uhispania | 301 |
| 5 | Japan | 511 |
| 6 | Qatar | 228 |
| 7 | Omani | 135 |
| 8 | Kuwait | 133 |
| 9 | Singapore | 60 |
| 10 | Ujerumani | 115 |
| 11 | Malaysia | 95 |
| 12 | Bahrain | 79 |
| 13 | Nepal | 55 |
| 14 | Ugiriki | 54 |
| 15 | Nyinginezo | 323 |
| | **Jumla kuu** | **4,545** |





**Chanzo:** Cashewnutinformation

### 2.3. Hali ya Soko la Korosho katika Nchi ya Vietnam

Nchini Vietnam bei ya korosho ghafi kutoka Afrika imeshuka kwa Dola za Kimarekani 20 hadi 30 kwa tani ikilinganishwa na mwezi Machi. Soko la korosho karanga bado halijatengamaa huku kukiwa na ongezeko la uingizaji wa korosho karanga kutoka nchi za Afrika na kuathiri wawekezaji wa ndani. Kulingana na VINACAS (Vietnam Cashew Association), katika miezi miwili ya kwanza ya 2023 pekee, zaidi ya tani 10,000 za korosho karanga ziliingizwa kutoka nje. Kwa mwaka mzima wa 2022 zaidi ya tani 78,000 za korosho karanga ziliingizwa kutoka nje.

**Jedwali Na.4: Bei za Korosho Ghafi katika Nchi ya India na Vietnam Aprili, 2023**

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI DUNIANI (INDIA NA VIETNAM) KWA KIPINDI CHA OKTOBA, 2022 HADI APRILI, 2023 | | |
|---|---|---|
| TAREHE | BEI-CIF USD/TON | |
| | BEI YA CHINI | BEI YA JUU |
| 31 Oktoba, 2022 | 1,050 | 1,280 |
| 05 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 27 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 12 Desemba, 2022 | 1,100 | 1,330 |
| 24 Desemba, 2022 | 1,150 | 1,320 |
| 14 Januari, 2023 | 1,200 | 1,275 |
| 28 Januari, 2023 | 1,250 | 1,390 |
| 18 Februari, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 13 Machi, 2023 | 1,150 | 1,165 |
| 24 Aprili, 2023 | 1,040 | 1,080 |
| SOT: 48-49 | | |




**Chanzo:** Cashewnutinformation



## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI DUNIANINCHI MBALIMBALI DUNIANI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji, viwango vya ubora pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

### 3.1 Bei ya Korosho Karanga Vietnam Kufikia Aprili, 2023

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini ikilinganishwa na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Kuna mabadiliko madogo ya bei kwa mwezi Aprili kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 5

**Jedwali Na. 5: Bei za Korosho Karanga Nchini Vietnam hadi kufikia Aprili, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA APRILI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | WW180 | 7.72 | 8.38 | 17,949.00 | 19,483.50 |
| White Whole Cashews 210 | WW210 | 6.84 | 7.28 | 15,903.00 | 16,926.00 |
| White Whole Cashews 240 | WW240 | 5.84 | 6.28 | 13,578.00 | 14,601.00 |
| White Whole Cashews 320 | WW320 | 5.51 | 5.84 | 12,810.75 | 13,578.00 |
| Large Pieces | LP | 3.31 | 3.64 | 7,695.75 | 8,463.00 |
| Small Pieces | SP | 2.43 | 2.87 | 5,649.75 | 6,672.75 |

**Chanzo:** Cashewinformation

### 3.2 Bei ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Magharibi Hadi Kufikia Aprili, 2023

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni pamoja na Ivory Coast, Ghana na Benin ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 6

**Jedwali Na. 6: Bei ya Korosho Karanga Afrika Magharibi hadi Kufikia Aprili, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA APRILI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | | | | |
| White Whole Cashews 210 | W210 | 8.16 | 8.49 | 18,972.00 | 19,739.25 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.95 | 6.17 | 13,833.75 | 14,345.25 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.62 | 5.95 | 13,066.50 | 13,833.75 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.29 | 5.62 | 12,299.25 | 13,066.50 |
| White Splits | WS | 4.63 | 4.74 | 10,764.75 | 11,020.50 |
| Large Pieces | LP | 3.97 | 4.30 | 9,230.25 | 9,997.50 |
| Small Pieces | SP | 2.98 | 3.42 | 6,928.50 | 7,951.50 |

**Chanzo:** Cashewinformation



### 3.3 Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi Hadi Kufikia Aprili, 2023

Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje katika nchi za Uholanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni nk. Ni kama ilivyo katika jedwali Na. 7


**Jedwali Na. 7: Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi hadi kufikia Aprili, 2023.**

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA APRILI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | 8.00 | 8.50 | 18,600.00 | 19,762.50 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 7.30 | 7.50 | 16,972.50 | 17,437.50 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 6.80 | 7.00 | 15,810.00 | 16,275.00 |
| White Splits | WS | 3.93 | 4.54 | 9,137.25 | 10,555.50 |
| Large White Pieces | LWP | 3.93 | 4.54 | 9,137.25 | 10,555.50 |

**Chanzo:** TACP

**Jedwali Namba 8: Uwiano Wa Bei Daraja WW320**

| UWIANO WA BEI DARAJA LA WW320 FOB | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Nchi | Bei ya Chini Dola/Kilo | Bei ya Juu Dola/Kilo | Bei ya Chini Tzs/Kilo | Bei ya Juu Tzs/Kilo |
| Vietnam | 5.51 | 5.84 | 12,810.75 | 13,578.00 |
| Afrika Magharibi | 5.62 | 5.95 | 13,066.50 | 13,833.75 |
| Tanzania | 6.80 | 7.00 | 15,810.00 | 16,275.00 |




**Chanzo: Bodi ya Korosho**

## 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2022/2023 ni tani 187,848.917 zenye thamani ya shilingi 345,832,150,275 ambapo tani 176,686.889 zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada zenye thamani ya shilingi 328,264,230,845. Mauzo ya korosho kupitia soko la awali hadi kufikia wiki ya mwisho ya mwezi wa Aprili ni tani 4,485.534 zenye thamani ya shilingi 7,553,178,250 na korosho zilizobanguliwa na wabanguaji wadogo ni takribani tani 1,483.665 sawa na tani 6,676.494 za korosho ghafi zenye makadirio ya thamani ya shilingi 10,014,741,180. Ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji unaendelea.



**Jedwali Na. 9a: Taarifa ya Uzalishaji Korosho Msimu wa 2022/2023 Hadi Kufikia Mwezi Aprili, 2023**

| TAARIFA YA UZALISHAJI KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 HADI KUFIKIA TAREHE 30/04/2023 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SN | MKOA | CHAMA KIKUU | GHALA ZA MNADA (KG) | THAMANI GHALA ZA MNADA (TSHS) | SOKO LA AWALI (KG) | THAMANI SOKO LA AWALI (TSHS) | ZILIZOBANGULIWA (KG) | | THAMANI UWIANO WA GHAFI (TSHS) |
| | | | | | | | ZILIZOBANGULIWA | UWIANO WA GHAFI | |
| 1 | MTWARA | TANECU | 33,518,494.00 | 63,447,865,104.00 | 1,486,294.00 | 2,411,476,400.00 | 893,156.00 | 4,019,202.00 | 6,028,803,000.00 |
| | | MAMCU | 59,609,667.00 | 111,449,764,229.00 | 931,022.00 | 1,571,913,400.00 | 116,881.00 | 525,964.50 | 788,946,750.00 |
| 2 | LINDI | RUNALI | 42,440,859.00 | 81,187,464,564.00 | 7,200.00 | 11,520,000.00 | 2,611.00 | 11,749.50 | 17,624,250.00 |
| | | LINDI MWAMBAO | 14,622,801.00 | 25,590,331,828.00 | 487,780.00 | 848,494,500.00 | 195,453.56 | 879,541.02 | 1,319,311,530.00 |
| 3 | RUVUMA | TAMCU | 15,156,209.00 | 26,809,585,960.00 | 126,446.00 | 191,965,000.00 | | - | - |
| 4 | PWANI | CORECU | 10,759,505.00 | 18,796,294,846.00 | 1,415,619.00 | 2,468,173,500.00 | 269,043.00 | 1,210,693.50 | 1,816,040,250.00 |
| 5 | TANGA | TACACU | 339,519.00 | 569,336,325.00 | | | 6,520.80 | 29,343.60 | 44,015,400.00 |
| 6 | SINGIDA | CEAMCU | | | 18,769.00 | 30,968,850.00 | | - | - |
| 7 | MOROGORO | MOFACU | 153,959.00 | 264,846,120.00 | | | | - | - |
| 8 | TABORA | | | | 2,000.00 | 3,000,000.00 | | - | - |
| 9 | DODOMA | DOMASIKA | 24,079.00 | 40,164,540.00 | | | | - | - |
| 10 | MBEYA | TAMCU | 25,850.00 | 45,418,450.00 | 404.00 | 666,600.00 | | - | - |
| 11 | NJOMBE | TAMCU | 35,947.00 | 63,158,879.00 | | | | - | |
| 12 | KIGOMA | | | | 10,000.00 | 15,000,000.00 | | - | - |
| | JUMLA NDOGO | | 176,686,889.00 | 328,264,230,845.00 | 4,485,534.00 | 7,553,178,250.00 | 1,483,665.36 | 6,676,494.12 | 10,014,741,180.00 |
| | JUMLA KUU UZALISHAJI | | | | | | | | 187,848,917.12 |
| | JUMLA KUU THAMANI | | | | | | | | 345,832,150,275.00 |

*NB: Taarifa hii ya uzalishaji ni hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023. Ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji bado unaendelea.*

**Jedwali Na. 9b: Korosho Zilizouzwa Kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.**

| Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani hadi Aprili, 2023) | | |
|---|---|---|
| KIPINDI CHA | KIASI KILICHOUZWA (KG) | THAMANI (TZS) |
| Mwezi Aprili | NA | NA |
| Jumlishi Oktoba-Februari | 176,686,889 | 328,264,230,845 |
| Jumla | 176,686,889 | 328,264,230,845 |

**Jedwali Na. 9c: Muhtasari Bei za Korosho Ghafi Katika Minada**

| Muhtasari Bei za Korosho Ghafi Katika Mnada | | | |
|---|---|---|---|
| Mwezi Uliopita (Machi, 2023) | | Mwezi wa Sasa (Aprili, 2023) | |
| Mwenendo wa Bei | Mwezi | Daraja la Kawaida | |
| | | Bei ya Juu | Bei ya Chini |
| | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,720 | 1,720 |
| | *Mabadiliko (%)* | | |

**Jedwali Na. 9c Bei za Mauzo ya Korosho Ghafi Kimkoa.**

| Bei ya Mauzo Korosho Ghafi ya Mkoa (Aprili, 2023) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MKOA** | **CHAMA KIKUU** | **MWEZI** | **Daraja la Kawaida** | |
| | | | **Bei ya Juu** | **Bei ya Chini** |
| **MTWARA** | **MAMCU** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,705 | 1,680 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |
| | **TANECU** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,605 | 1,604 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |
| **LINDI** | **RUNALI** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,770 | 1,600 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |
| | **LINDI MWAMBAO** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,726 | 1,726 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |
| **PWANI** | **CORECU** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,520 | 1,520 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |
| **RUVUMA** | **TAMCU** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,605 | 1,605 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |
| **MOROGORO** | **MOFACU** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,721 | 1,721 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |
| **TANGA** | **TACACU** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,719 | 1,719 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |
| **DODOMA** | **DOMASIKA** | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,720 | 1,720 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |

Alama (▲▼►) zinaonyesha mwelekeo wa mabadiliko ya bei. (▲) Bei imeongezeka; (▼) Bei imeshuka; (►) Hakuna mabadiliko ya bei.

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania
2023

## 5.0 MAANDALIZI YA MBIO ZA KOROSHO (KOROSHO MARATHON) MSIMU WA 2023/2024

Bodi ya Korosho inaendelea na maandalizi ya mbio za korosho (Korosho Marathon) msimu wa pili. Uzinduzi wa mbio hizo utafanyika tarehe 13 Mei, 2023 kwa kugawa mashine mia moja (100) za kubangua korosho kwa vikundi vidogo vya ubanguaji wa korosho vya mkoa wa Mtwara na Lindi. Zoezi hili litafanyika katika mji wa Tandahimba na kufuatiwa na uzinduzi rasmi utakaofanyika katika hoteli ya Luwa Evergreen mjini Mtwara. Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika tarehe 2 Septemba, 2023 katika uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara na malengo ya mbio hizo ni kuhamasisha ulaji wa korosho karanga na matumizi ya bidhaa zinazotokana na korosho nchini.

## 6.0 MKUTANO WA KIMATAIFA WA KOROSHO 2023

Tanzania ikiwa ni mojawapo ya nchi zinazoongoza kwa uzalishaji korosho duniani, huku ikishika nafasi ya pili katika bara la Afrika na nafasi ya sita duniani kwa mujibu wa taarifa za African Cashew Alliance (2021). Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea na maandalizi ya mkutano wa kimataifa wa korosho nchini utakaoitwa “Tanzania International Cashew Conference” kuanzia tarehe 11 Oktoba, 2023 hadi 14 Oktoba, 2023, katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere.

Lengo la mkutano huo ni kuhamasisha maendeleo ya zao la korosho kwa kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika zao la korosho. Kupitia mkutano huo, inatarajiwa ushiriki wa wadau mbalimbali katika Nyanja za utafiti, utengenezaji mashine za usindikaji, viwanda vya ubanguaji na uwekezaji. Mkutano huo utaenda sambamba na maonyesho ya bidhaa zitokanazo na zao la korosho na teknolojia mbalimbali zitumikazo katika usindikaji wa bidhaa za korosho.

## 7.0 ZOEZI LA UHUISHAJI WA KANZIDATA YA WAKULIMA WA ZAO LA KOROSHOKOROSHO

Bodi ya korosho kwa kushirikiana na Halmashauri zinazolima zao la korosho inaendelea na zoezi la kuhuisha kanzi data ya wakulima wa korosho. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili tayari manispaa ya Mtwara Mikindani, Halmashauri ya wilaya ya Mtwara, Halmashauri ya wilaya Nanyamba na Halmashauri ya wilaya Tandahimba zimehuisha kanzi data za wakulima. Zoezi bado linaendelea na mpaka sasa jumla ya wakulima 109,033 wamefikiwa na kuhuishwa taarifa zao katika halmashauri nne kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Taarifa ya Mwenendo wa Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa Korosho Kufikia Tarehe 30/04/2023.** 2023.

| Na. | Halmashauri | Idadi ya Wakulima Waliofikiwa |
|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Mtwara | 1,937.00 |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya Mtwara | 15,790.00 |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya Nanyamba | 26,591.00 |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya Tandahimba | 64,715.00 |
| | **Jumla** | **109,033.00** |

**8.0 TAARIFA YA MAPOKEZI YA PEMBEJEO ZA KOROSHO KWA MSIMU WA MWAKA 2023/2024**

Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea na upokeaji wa pembejeo za zao la korosho kwa ajili ya msimu wa 2023/2024. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili tayari jumla ya lita 776,990 za viuatilifu vya maji, Sulphur ya unga tani 1,052.850 na mabomba 5,000 kwa ajili ya upuliziaji tayari vimeshapokelewa katika ghala za kukusanyia zilizopo Mtwara. Aidha, vituo vingine vya kupokelea pembejeo viko katika Mikoa ya Pwani na Lindi.







| TAARIFA YA MAPOKEZI YA VIUATILIFU NA MABOMBA MSIMU WA 2023/2024 HADI KUFIKIA 30/04/2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **MZABUNI** | **KIUATILIFU/PEMBEJEO** | **KIUATILIFU CHA MAJI (LITA)** | **SULPHUR YA UNGA (KG)** | **KISUMBUFU DHIBITIWA** |
| 1 | BENZ AGRO | INDAZOLE | 164,460.00 | | Ubwiri Unga na Ugonjwa wa Blaiti |
| | | BENSVIL 5SC | 37,540.00 | | Ubwiri Unga |
| 2 | MERU | PACHA | 150,000.00 | | Ubwiri Unga na Ugonjwa wa Blaiti |
| | | METAX | 200,000.00 | | Ubwiri Unga na Ugonjwa wa Blaiti |
| | | AGROZEB GOLD | 100,000.00 | | Ubwiri Unga |
| 3 | SUBA AGR | SUBATEX | 124,990.00 | | Ubwiri Unga na Ugonjwa wa Blaiti |
| 4 | TPM | SULPHUR | | 699,625.00 | Ubwiri Unga |
| 4 | BAJUTA | SULPHUR | | 353,225.00 | Ubwiri Unga |
| **JUMLA** | | | **776,990.00** | **1,052,850.00** | |
| 5 | FAHAMU | MABOMBA (IDADI) | 2,000.00 | | Upuliziaji na Unyunyiziaji |
| | MERU | MABOMBA (IDADI) | 3,000.00 | | Upuliziaji na Unyunyiziaji |
| **JUMLA** | | | **5,000.00** | | |




MAWASILIANO:
MKURUGENZI MKUU
BODI YA KOROSHO TANZANIA
S.L.P 533 TANU ROAD – MTWARA
Simu: +255 (23) 233 3303/233 3450
Barua pepe: info@cashew.go.tz
Tovuti: www.cashew.go.tz